
**KENYA NATIONAL EXAMINATION COUNCIL
REVISION MOCK EXAMS 2016
TOP NATIONAL SCHOOLS**

**KENYA HIGH SCHOOL
KISWAHILI
KARATASI YA 3**

SCHOOLS NET KENYA
Osiligi House, Opposite KCB, Ground Floor
Off Magadi Road, Ongata Rongai | Tel: 0711 88 22 27
E-mail: infosnkenya@gmail.com | Website: www.schoolsnetkenya.com

KENYA HIGH SCHOOL KCSE TRIAL AND PRACTICE EXAM 2016

102/3

FASIHI

KARATASI YA TATU

SEHEMU A

1. Swali la lazima

Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yafuatayo

1. Ningali kindi nishike, viungo vi teketeke,
Sinipe simi nizuke, na vichaka nivifyeke,
Dhibiti nivuvumke, usidiriki makekeke,
Pulika usikiuke, mpe mtoto hakiye,
 2. Mungavunja haki yake, madhara milele kwake,
Wa kiume na wa kike, mpeni yaliyo yake,
Kwa makini mumshike, kadiri makamo yake,
Pulika msikiuke mpe watoto haki yake.
 3. Kwanza ni watani wake, Uandae aridhike,
Atuze mtima wake, maudhi yasimshike,
Kuta nne zizunguke, na hofu imbanduke,
Pulika msikiuke, mpe mtoto haki yake.
 4. Pili ni chakula chake, 'jengeke siha yake,
Mpe titi alishike, anyonye asihinike,
Kuta nne zizunguke, na hofu imbanduke,
Pulika msikiuke, mpe mtoto haki yake.
 5. Mpe tiba 'sidhurike, ndwele asiathirike,
Fikira zimpanuke, atambue rika lake,
Penye daraja avuke, mvushe asighurike,
Pulika msikiuke, mpe mtoto haki yake.
 6. Angakuwa chekecheke, apande shule avuke,
Mpe taaluma yake, adhibiti apanuke,
Ufundi na dhima zake, ayashike ajivike,
Pulika msikiuke, mpe mtoto hakiye.
 7. Jifanye kipenzi chake, mpende asihinike,
Amani ijae kwake, daima asikereke,
Vizito usimtwike, visivyo vipimo vyake,
Pulika msikiuke, mpe mtoto hakiye.
 8. Elimu chuo ashike, apanuke bongo lake,
Atende jukumu lake, ahudumie wenzake,
-

Ajue wajibu wake, atende asitepweke,
Pulika msikiuke, mpe mtoto hakiye.

9. Hima kwa Muumba wake, muhimidi aongoke,
Roho yake isafike, ahera asisumbuke,
Neema imzunguke, maovu yamuepuke,
Pulika msikiuke, mpe mtoto hakiye.

Maswali

- a) Nafsi neni ametaja haki zinazomstahiki mtoto. Zitaje na uzifafanue (alama 4)
- b) Eleza kwa kutoa mifano mbinu mbili zinazotumiwa na mshairi kutosheleza mahitaji ya kiarudhi
- c) Bainisha umuhimu wa tamathali zozote mbili za usemi zilizotumika katika shairi hili
(alama 4)
- d) Eleza ubeti wa tano kwa lugha nathari (alama 4)
- e) Taja na ufafanue toni ya mshairi (alama 2)
- f) Eleza maana ya misamiati ifuatayo (alama 2)
- i) Mtima
 - ii) Asihinike
 - iii) mbi
 - iv) asighurike

SEHEMU B

TAMTHILIA: Timothy Arege: Mstahiki Meya

Jibu swali la 2 au 3

2. "Mtu huvuna alichopanda. Ukipanda pojo huweza kuvuna kunaziu"
- a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
 - b) Thibitisha kuwa warejelewa walikuwa wamepanda pojo (alama 10)
 - c) Eleza sifa za mnenewa (alama 6)
3. Tamthilia ya Mstahiki Meya inamulika na kupiga vita utawala dhalimu katika mataifa ya kiafrika. Jadili (alama 20)

SEHEMU C

RIWAYA: Ken Walibora: Kidagaa Kimemwozea

Jibu swali 4 au 5

4. “Aliwaonea gere wanawake wengine katika eneo la Sokomoko waliovaa rinda moja.....”

a) Weka dondoo hili katika muktadha wake (alama 4)

b) Eleza sifa na umuhimu wa anayemfanya mrejelewa kuwaonea wanawake wengine gere (alama 10)

c) Jadili maudhui matatu yanayodokezwa katika dondoo hili (alama 6)

5. “Mla naye huliwa zamu yake ifikapo.”

Thibitisha kauli hii kwa kuirejelea riwaya ya kidagaa kimemwozea. (alama 20)

SEHEMU D:

HADITHI FUPI: Ken Walibora : *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*

Jibu swali la 6 au 7

6. Onyesha jinsi swala la ubaguzi linavyodhihirika katika hadithi zozote nne(alama 20)

7. “Hawakurudhisha macho tu, bali pia walicheza michezo ya ujana ama wakijua au kutojua kuwa ujana una tegemeo.”

a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)

b) Dhihirisha namna ‘Michezo ya ujana’ ya wanaorejelewa ilivyosambaratisha tegemeo la ujana wao. (alama 8)

c) Jadili ukweli wa kauli kwamba, “Tamaa mbele mauti nyuma” ukirejelea hadithi ya “Tazamana na mauti” (alama 8)

SEHEMU E

FASIHI SIMULIZI

8. a) Eleza sifa nne za ushairi simulizi (alama 8)

b) Taja na uelezee aina tatu za magizo (alama 6)

c) Jadili mbinu nne za kimtindo za methali huku ukitoa mifano mwafaka (alama 4)

d) Eleza umuhimu wa hekaya katika jamii (alama 4)